

# JIMBO KUU KATOLIKI LA DAR ES SALAAM

**PAROKIA YA KUNG'ARA KWA YESU KRISTO, MBEZI MSHIKAMANO**

S.L.P. 280 D'SALAAM, +255 686 794177, E: katolikimshikamano@gmail.com



## MATANGAZO - SHEREHE YESU KRISTO MFALME - 23.11.2025

| | | |
|---|---|---|
| 1. | LEO DOMINIKA 23.11.2025 | **SHEREHE YA BWANA WETU YESU KRISTO MFALME**<br>**SIKUKUU YA VIJANA ULIMWENGUNI**<br>Mchango wa pili ni kwa ajili ya Ujenzi |
| 2. | JUMAMOSI 29.11.2025 | Kutakuwa na Misa ya kuhitimisha matembezi ya Sanamu ya Bikira Maria katika **Kanda J** saa 10:00 jioni na kukabidhi Sanamu kwa **Kanda K**. Jumuiya zihimize na kufuatilia bahasha za Kapu la Mama na kuzirejesha katika Misa za kuhitimisha matembezi ya sanamu. |
| 3. | WARSHA YA WAAMINI WOTE JIMBO | Warsha ya waamini wote wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam itafanyika Jumamosi ijayo 29.11.2025 katika viwanja vya Parokia ya Kristo Mfalme Tabata kuanzia saa 2:00 asubuhi. Kutakuwa na Mada mbili,<br>1. Uchaguzi/Uongozi katika Kanisa 2. Mwaka wa Jubilei Kuu<br>Kutakuwa pia na vyeti kwa wenye Jubilei za miaka 25, 50 na 75.<br>**Sasa ada ya ushiriki imeondolewa, ushiriki ni bure, tujiandikishe kwa wingi. Watakaoshiriki watachangia nauli sh. 5,000/=.**<br>***Kila Jumuiya inatakiwa kuwasilisha taarifa ya maendeleo ya uandikishaji washiriki wa Warsha kwani inatakiwa Jimboni.***<br>*Watakaoenda wanaomba kuthibitisha kwa kujiandikisha ofisini kabla ya Jumatano 26.11.2025* |
| 4. | UCHAGUZI WA VMJ PAROKIA | Uchaguzi wa Kamati Tendaji wa Vyama wa Kitume ngazi ya Parokia vya Lejio Maria, Utoto Mtakatifu, Karismatiki Katoliki, CPT na Viwawa utafanyika Dominija ijayo 30.11.2025.<br>Pia leo utafanyika uchaguzi wa Wazee na Wastaafu, Moyo Mtakatifu wa Yesu na St. Vicent. |
| 5. | DOMINIKA 30.11.2025 | **DOMINIKA YA 1 YA MAJILIO MWAKA A**<br>**Misa ya 1: Saa 12:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Jumuiya ya Mt. Gasper Del Bufalo<br>Watangaza Neno: Pancracia Shirima na Elizabeth Machange<br>**Misa ya 2: Saa 2:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Jumuiya ya Mt. Yohane Maria Vianey<br>Watangaza Neno: Scolastica Mwenda na Pius Laswai<br>**Misa ya 3:** Misa ya watoto Wasimamiazi ni Mt. Gasper Del Bufalo na Mt. Yohane Maria Vianey<br>**Kila Jumuiya inakumbushwa kuleta majina ya watoto**<br>**Mchango wa Pili ni kwa ajili ya Ujenzi** |

| | | |
|---|---|---|
| 6. | BAHASHA ZA MFUKO WA UINJILISHAJI - PAPA | Tumepokea bahasha za Marafiki wa Mashirika ya Uinjilishaji ya Baba Mtakatifu (PMS), kila Jumuiya iligawiwa kati ya Bahasa 2 au 3 Dominika iliyopita. Ambao bado hawajachukua wanaombwa kuchukua leo. Mwisho wa kurejesha ni Dominika ijayo 30.11.2025. |
| 7. | KUWAOMBEA MAREHEMU | Mwezi Novemba ni mwezi wa kuwakumbuka na kuwaombea marehemu wetu. Fomu za kuwaombea zimetolewa na tutatakiwa kuweka sadaka ya nia ya kuwaombea katika Misa. Fomu na sadaka ziwekwe kwenye bahasha na kufungwa. |
| 8. | MKUTANO WA H/W PAROKIA | Mkutano wa H/W Parokia utafanyika Dominika ya 07.12.2025 mara baada ya Misa ya Kwanza. Wahusika ni viongozi wa Kamati Tendaji za Jumuiya na weyeviti wa VMJ ngazi ya Parokia. |
| 9. | UWAKA DAY | Uwaka Day Parokia itaanzimishwa Jumamosi ya 06.12.2025 hapa Parokiani na itaanza kwa Misa Takatifusaa 3:00 asubuhi. Wanaumwe wote wanaombwa kushiriki katika maandalizi na siku hiyo. |
| 10. | WAWATA | Hija ya Wawata wote Bagamoyo 06.12.2025. Watakaoshiriki wajiandikishe kwa viongozi wa Wawata wa Jumuiya na Parokia. Nauli ni **Shs. 10,000.** |
| 11. | HUDUMA YA MACHO | Kutakuwa na huduma ya kupima macho hapa Parokiani Dominika ijayo 30.11.2025 mara baada ya Misa ya kwanza mpaka saa 7:00 mchana. Gharama ya kupima ni **Shs. 3,000** na Miwani ni kuanzia **Shs. 15,000** na kuendelea kutegemea aina ya Miwani. |
| 12. | CHAKULA KWA WAHITAJI | Chakula kwa wahitaji kitatolewa Jumanne 25.11.2025 saa 10:00 jioni. Wahusika wanaombwa kufika kwa wakati. |
| 13. | GAZETI LA TUMAINI LETU | Viongozi wa Jumuiya wanakumbushwa kuchukua GAzeti la Tymaini letu ofisini na kufanya malipo ya nakala 4 kati ya 5. |

***Kauli Mbiu ya Mwaka wa Jubilei Kuu: "Jubilei 2025 – Mahujaji wa Matumaini."***

## MATEMBEZI YA SANAMU YA BIKIRA MARIA KATIKA MWEZI WA ROZARI NA KAMPENI YA KAPU LA MAMA MARIA 2025

| WIKI | TAREHE | KANDA HUSIKA | MSA YA HITIMISHO |
|---|---|---|---|
| 1 | 28/09 - 04/10 | A | SAA 1:00 ASUB |
| 2 | 04/10 – 11/10 | B | SAA 1:00 ASUB |
| 3 | 11/10 – 18/10 | C | SAA 1:00 ASUB |
| 4 | 18/10 – 25/10 | D & E | SAA 1:00 ASUB |
| 5 | 25/10 – 01/11 | F & G | SAA 1:00 ASUB |
| 6 | 01/11 – 08/11 | H | SAA 1:00 ASUB |
| 7 | 08/11 – 15/11 | I | SAA 1:00 ASUB |
| 8 | 15/11 – 22/11 | J | SAA 10:00 JIONI |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 9 | 22/11 – 29/11 | K | SAA 10:00 JIONI |

**TANGAZO LA DARAJA YA UPADRE KWA MARA YA TATU**

Mhashamu Sana Askofu Mkuu Jude Thaddeus Ruwa'ichi OFMCap wa Jimbo Kuu la DSM anatangaza **Daraja ya Upadri** wa Shemasi **Nicholaus Paschal Nkoronko**, **SDS** wa Shirika la Mungu Mwokozi - Wasalvatoriani kutoka Parokia ya Kigamboni katika Jimbo Kuu la Dar es Salaam, anayetarajiwa kupewa Daraja Takatifu ya Upadri tarehe 29.11.2025 katika Kanisa la Mt. Yakobo Mtume, Nyumba ya Masista Wasalvatoriani - Migongo, Jimbo la Tunduru Masasi.

**MASOMO DOMINIKA – DOMINIKA YA 1 YA MAJILIO MWAKA A - 30.11.2025**

| | |
|---|---|
| SOMO I | Isa.2:1-5 |
| WIMBO WA KATIKATI | Zab 122:1-4, 8-9 |
| SOMO II | Rum.13:11-14 |
| SHANGILIO | Zab. 85:7 |
| INJILI | Mt.24:37-44 |